JAMHULI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAISI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (OR-TAMISEMI)

HALMASHAURI YA WILAYA YA MTWARA

***NAMBA ZA SIMU***

***Mkuu wa Shule 0788590514***
***Makamu Mkuu wa Shule (Utawala) 0759516187***
***Makamu Mkuu wa Shule (Taaluma) 0786804745***
***Mwalimu wa Malezi (Matron) 0623993013***

***SHULE YA SEKONDARI MUSTAFA SABODO, S.L.P 158 MTWARA***

MZAZI/MLEZI WA: ………………………………………………………………

**YAH; MAELEKEZO UA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA SEKONDARI MUSTAFA SABODO MWAKA 2026**

**Tafadhali rejea somo tajwa hapo juu**

Ninayo furaha kukufahamisha kuwa mtoto wako ………………………………………………………………

Ni miongoni mwa Wanafunzi wachache waliopata fursa ya kuendelea na masomo ya kidato cha kwanza katika Shule ya sekondari Mustafa sabodo – Hongera sana kwa fursa hiyo. Kwa barua hii nakuletea fomu ya kujiunga na Shule ya Sekondari Mustafa Sabodo kwa mwanao.

Tafadhali nakuomba wewe na mwanao msome maelekezo haya kwa kina na kisha mkamilishe yale yote yanayotakiwa. Pamoja na kuyasoma kwa kina naomba uendelee kumshauri mwanao juu ya kutumia nafasi hii aliyoipata vema ili lengo na azma yake itimie. Nakutakia maandalizi mema na karibu sana Mustafa Sabodo Sekondari.

Wako

KHAJI S. NYENGEDI

MKUU WA SHULE

HALMASHAURI YA WILAYA YA MTWARA
SHULE YA SEKONDARI MUSTAFA SABODO

SIMU 0788590514

***S.L.P 158***
***MTWARA***

KUMB. NA. MSS/A.01/ 2026

Tarehe _____________

Ndg. Mzazi/Mlezi wa -----------------------------------------------------------------

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE**

MZAZI/MLEZI WA: ……………………………………………………………………………………

Ninayo furaha kukujulisha kwamba mtoto wako …………………………………………………………

Ni miongoni mwa Wanafunzi walioteuliwa kujiunga na Shule ya Sekondari **MUSTAFA SABODO** kidato cha kwanza 2026. Shule ipo Mkoa wa Mtwara, Wilaya ya Mtwara, umbali wa **km 17** kutoka Mtwara mjini kwenye barabara iendayo **Masasi** na **Lindi**. Usafiri wa basi/daladala unapatikana kwa urahisi kutoka stendi kuu Mtwara

Anatakiwa kufika hapa shuleni tarehe **05/01/2026** bila kukosa. Aidha mwanao atajiunga na shule hii baada ya kutekeleza masharti yafuatayo:-

**(a) AFYA**

Awasilishe hapa shuleni fomu **"request for medical Examination"** iliyojazwa na daktari yeyote wa hospitali ya serikali baada ya kupimwa. Fomu hiyo imeambatanishwa na barua hii.

**(b) SARE YA SHULE**

**C 1. WASICHANA**

1. Awe na sketi mbili rangi ya bluu bahari rinda box **(urefu wake ukaribie fundo la miguu)** na shati mbili nyeupe mikono mifupi. Au nusu kanzu mbili nyeupe zisizobana, mikono mirefu na juba mbili rangi nyeupe za kushonwa na kofia nyeupe ya kichwani.
2. Sweta rangi ya bluu.
3. Awe na jozi mbili za viatu vya ngozi vyeusi vya kamba, viwe na visigino vifupi.
4. Awe na jozi mbili(2) za soksi nyeupe, ziwe ndefu (stoking)
5. Sketi mbili nyeusi rinda box **(urefu wa sketi ukaribie kwenye fundo la miguu)**
6. T-shirt 2 za bluu **zinapatikana shuleni zenye nembo ya shule** kwa ajili ya kushindia na kazi za nje au nusu kanzu mbili za blue zisizobana, mikono mirefu na juba mbili rangi ya blue za kushonwa na kofia ya blue ya kichwani.
7. Awe na nguo za ndani za kutosha pamoja na taulo za kike (pedi) za kutosheleza muhula mzima

**C 2. WAVULANA**

(i) Awe na suruali mbili rangi ya bluu bahari zilizoshonwa kiheshima (zisishonwe katika mtindo wa jeans na zisibane)
(ii) Sweta rangi ya bluu.
(iii) Awe na mashati mawili meupe ya mikono mifupi isiyobana
(iv) Awe na jozi mbili (2) za soksi nyeupe
(v) Awe na jozi mbili (2) za viatu vyeusi vya kamba, viwe na visigino vifupi
(vi) Suruali 2 nyeusi zilizoshonwa kiheshima (zisishonwe katika mtindo wa jeans na zisibane)
(vii) T-shirt 2 **zinapatikana shuleni zenye nembo ya shule** za bluu kwa ajili ya kushindia na kazi za nje
(viii) Awe na mkanda mweusi wa ngozi.

**MUHIMU SANA: Suruali ziwe za rinda na zenye upana wa nchi 8 na zitahakikiwa.**

- ***Nguo zingine tofauti na zilizoainishwa katika fomu hii haziruhusiwi na hivyo mwanafunzi hatakiwi kuja nazo.***
- ***BIMA KUBWA ya Afya ni ya LAZIMA kuja nayo pindi tu anapofika shuleni ili kurahisisha huduma ya matibabu kwa mwanafunzi.***

**ZINGATIA:**

(i) Tafadhali, mwanao anapaswa asome sheria, kanuni na taratibu za Shule na kama yuko tayari kufuata taratibu husika akiri mbele yako kwa kujaza fomu husika zilizoambatanishwa

(ii) Mwanafunzi atakae chelewa kufika Shuleni zaidi ya tarehe ya kuripoti shuleni **hatapokelewa**. Hivyo ni vyema ukamwandaa mapema mwanao na akafika mapema Shuleni.

(iii) **SI RUHUSA** kwa Mwanafunzi kumiliki **SIMU** awapo Shuleni na endapo atabainika/atakamatwa na **SIMU** atasimamishwa/atafukuzwa Shule.

*Tafadhali, mwanafunzi afike Shuleni na barua hii na ajaze kwa ukamilifu sehemu ya taarifa zote maalum.*

*Nakutakia safari njema*

KARIBU SANA

KHAJI S. NYENGEDI

MKUU WA SHULE.

***NB: Kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambae ni mwanafunzi ni mgonjwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.***

***TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZILIZOPO HAPO JUU***

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MTWARA**

**SHULE YA SEKONDARI MUSTAFA SABODO**

## SHERIA ZA SHULE

Zifuatazo ni sheria za Shule kinyume nazo kutasababisha Mwanafunzi kuadhibiwa, kusimamishwa masomo au kufukuzwa Shule kabisa

## MAKOSA YA KUFUKUZWA SHULE

1. Wizi
2. Uvutaji wa sigara
3. Kupata ujauzito au kutoa mimba
4. Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa.
5. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
6. Kugoma na kuhamasisha mgomo
7. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla
8. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga Mwalimu au mtu yeyote kwa ujumla.
9. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yeyote yale yanayovunja sheria za nchi
10. Kudharau Bendera ya Taifa
11. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
12. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.
13. Kugoma na kuhamasisha mgomo
14. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo Shuleni.
15. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya. Kutoka nje ya Shule bila kibali/ruhusa
16. Kukataa adhabu kwa makusudi.
17. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya Shule.

***MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUADHIBIWA:***

1. Kutovaa sare sahihi
2. Kutowaheshimu wafanyakazi wote waliopo shuleni kama walezi wake.
3. Kutoonyesha dhamira ya kusaidia na kushiriki katika kazi kwani kazi ni kielezo cha utu
4. Kutoheshimu au kutothamini kazi za aina zote zinazotolewa na uongozi wa shule
5. Kuvaa mavazi yasiyo na heshima
6. Kutotii kengele au kushindwa kuitikia wito wa kiongozi aliyemuita
7. Kutoheshimu picha za viongozi wa Serikali, Nembo ya Taifa, Wimbo wa Taifa na Fedha za Taifa
8. Kutohudhuria vipindi vya darasani kwa muda wote wa masomo
9. Kushindwa kuthamini muda
10. Kutowahi katika shughuli zote kama zilizopangwa ukiwemo wito wa dharura
11. Kutohudhuria kazi zote za mikono, mikutano yote ya shule, ukaguzi na usafi
12. Kufuga ndevu na nywele
13. Kutovaa sare za shule katika sehemu zifatazo
    a. Darasani
    b. Shughuli za kishule nje ya shule
    c. Mhadhara wa shule (school baraza)
    d. Kwenda kutibiwa hospitalini
    e. Kwenye maandamano yaliyo rasmi
    f. Anaposafiri kwenda na kurudi likizo
14. Kuvaa kofia, viatu vya gorofa na mapambo yeyote kwa mfano pete, mkufu.
15. Kutokuwa msafi katika mwili na nguo
16. Kutoheshimu mipaka ya hule.
17. Marufuku kuingia sehemu zifuatazo bila ruhusa
    a. Ofisi ya walimu
    b. Ofisi za shule
    c. Maabara
    d. Jikoni
    e. Nyumba za walimu na wafanyakazi wasio walimu
18. Sehemu zifuatazo ni marufuku kabisa kutembelea
    a. Vilabu vya pombe
    b. Kumbi/nyumba za starehe na disco
    c. Nyumba za kufikia wageni (guest houses)

Yafuatayo ni baadhi ya mambo yanayoweza kusaidia kumfanya mwanafunzi kuwa nadhifu ***Kukata kucha, kunyoa ndevu (wavulana) kuvaa nguo safi na za heshima, kukata nywele na kuwa fupi, kutojirembesha na kutopaka madawa kwenye ngozi na nywele, kupiga viatu kiwi, kufunga mkanda.***

**ANGALIA KWA MAKINI:**

(i) Kila mzazi/ mlezi wa mwanafunzi azisome sheria / kanuni na taratibu kwa uangalifu.

(ii) Karatasi zilizoambatanishwa zishughulikiwe ipasavyo na zirejeshwe suleni zikiwa zimejazwa kwa ukamilifu.

**KHAJI S. NYENGEDI.**

**MKUU WA SHULE**

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION FORM.**

To be completed by a medical officer (NAME) ………………………………………………………………………………

Name of student……………………………………………………………………………………………………………..

Form ………………………………………………… Term ……………………….. Year …………………………………

Dear Doctor
Please kindly examine the above named student to prove his/her fitness undertaking studies at our school.

1. X-ray ( ) 2. Urine ( ) 3. Stool ( )

4. Physical fitness ( ) 5. V.D ( ) 6. Tuberculosis ( ) 7. Pregnancy ( )

A: (I) PRELIMINARY INFORMATION BY THE STUDENT BEFORE THE DOCTOR)

| NO | DISEASE | YES/NO | NO | DISEASE | YES/NO |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Tuberculosis | | 10 | Epilepsy | |
| 2 | Pneumonia | | 11 | Ear, Nose and threat | |
| 3 | Asthma | | 12 | Skin disorder disease | |
| 4 | Heart trouble | | 13 | Anemia | |
| 5 | Recurrent indigestion | | 14 | Operations | |
| 6 | Jaundice | | 15 | Serious Accident | |
| 7 | Dysentery | | 16 | Malaria | |
| 8 | Kidney and Urinary trouble | | 17 | Stomach trouble | |
| 9 | Nervous breakdown | | 18 | Eye disorder. | |

**(II) VACCINATION AND INNOVULATIONS HISTORY**

| **DISEASE** | **1ST DATE** | **2ND DATE** | **3RD DATE** |
|---|---|---|---|
| Small pox | | | |
| Whooping cough | | | |
| Measles | | | |
| Yellow fever | | | |
| Cholera | | | |

**Official**

B: MEDICAL EXAMINATION REPORT

a. Weight
b. Heat Beat
c. Vision etc

**MEDICAL CERTIFICATE**

I have examined the above and consider that he/she is physically fit/unfit to undergo studies. NAME OF THE EXAMINATION CENTRE…………………………………………………..
DOCTORS NAME & SIGNATURE ………………………………………………….
DATE ……………… OFFICIAL STAMP…………………SIMU:………………………..

**SHULE YA SEKONDARI MUSTAFA SABODO S L P 158. MTWARA**

**TAARIFA MUHIMU KUHUSU MWANAFUNZI MPYA.**

| PICHA |
|---|

**SEHEMU A.**

JINA LA MWANAFUNZI ……………………………………………………………………………………

wa kidato ………………………….. Mwaka ……………………………..

Dini …………………………………………………………………………………………………… ..

**ELIMU**

(i) Shule ya Msingi niliyosoma ni ………………………………………. iliyopo (Kata) ……………………………..

Wilaya ya ………………………………………………… Mkoa wa …………………………………………………………

kuanzia mwaka …………………………………………….. mpaka ……………………………………………………….

**SEHEMU B: TAARIFA ZA WAZAZI/WALEZI NA JAMAA:**

(i) Baba anaitwa ………………………………………………………………………………………………………..

Anaishi kijiji/mtaa ……………………………………………………… kata ………………………………………………

Kazi yake ni …………………………………………………….. na anwani yake ni …………………………………….

……………………………………………………………………………………………………………………………

Namba yake ya simu ni …………………………………………………………………………………………..

(ii) Mama yangu anaitwa ……………………………………………………………………………………………

Anaishi kijiji/mtaa ……………………………………………………… kata ………………………………………………

Kazi yake ni …………………………………………………….. na anwani yake ni …………………………………….

……………………………………………………………………………………………………………………………

Namba yake ya simu ni …………………………………………………………………………………………..

(iii) Jina kamili la Mzazi/Mlezi anayemuhudumia mwanafunzi ikiwemo kumpatia mahitaji yake Muhimu

……………………………………………………………………………………………………………………………

Uhusiano ……………………………………………………………………………………………………………..

Anuani Kamili ………………………………………………………………………………………………………….

Simu ……………………………………………………… Barua pepe ………………………………………………….

Kazi yake ……………………………………………………………………… Umri ………………………………………..

(iv) Uwepo wa Wazazi: Baba – YUPO HAI/AMEFARIKI. Kama amefariki ni lini? ...........................................

Mama – YUPO HAI/AMEFARIKI. Kama amefariki ni lini? ..........................................

(v) Majina na picha za watu wasiozidi watatu watakaoruhusiwa kumtembelea mwanafunzi

| | | |
|---|---|---|
| **PICHA 1** | PICHA 2 | PICHA 3 |

Jina Jina .................................. Jina ................................... Jina ........................................

uhusiano ................................. .. uhusiano ................................. uhusiano .................................

Simu .......................................... Simu ....................................... Simu ......................................

Mimi ………………………………………………………………….. ambae ni mwanafunzi wa kidato cha ………… katika mwaka wa masomo ..........................................nathibitisha kuwa maelezo yote niliyoyatoa hapo juu ni ya kweli na sahihi.

**SEHEMU C: UTHIBITISHO WA MWANAFUNZI**

Mimi.................................................................................................nakiri kuwa nimezisoma sheria, kanuni na taratibu za Shule kwa umakini na utulivu kubwa. hivyo basi ninaahidi “nitazifuata sheria, kanuni na taratibu za Shule kama zilivyoelekezwa. aidha ninaamini kuwa sheria na taratibu zote zipo kwa nia ya kunisaidia katika Nyanja zote muhimu ikiwa ni pamoja na nidhamu na taaluma”

kinyume na hivyo hatua stahiki za kinidhamu zichukuliwe dhidi yangu

jina la Mwanafunzi ………………………………………………………….. sahihi ……………………………………

jina la mzazi/mlezi ……………………………………………………….. Sahihi …………………………………..

Tarehe ……………………………………

MKATABA WA MAKUBALIANO KATI YA UONGOZI WA SHULE NA MZAZI KUHUSU MWENENDO WA KITAALUMA WA MWANAFUNZI SHULENI

Mkataba huu umeingiwa leo......................................Kati ya uongozi wa shule ya sekondari Mustafa sabodo na .........................................................................................ambaye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi ........................................................... (Taja jina ) ambaye amepokelewa akiwa kidato cha ……………………………

Kwamba mwanafunzi itampasa kusoma kwa juhudi kubwa ili kuweza kupata ufaulu ambao utamfanya mwanafunzi kusonga mbele zaidi kitaaluma.

Kwamba Mwanafunzi itampasa kuwa na ufaulu wa daraja la **kwanza**, na la **pili** tu wakati wote atakapokuwa shuleni na kwamba anashiriki katika kazi zote za ndani na nje ya darasa.

Kwamba endapo Mwanafunzi atashindwa kufikia ufaulu huo, uongozi wa Shule utakutaka mzazi umbadilishie Shule mwanao kwani atakuwa ameshindwa kwendana na malengo ya Shule

**KHAJI S. NYENGEDI**

**MKUU WA SHULE**

***MZAZI ANDIKA MAONI YAKO KUHUSU KUKUBALIANA NA MAELEKEZO YALIYOTOLEWA HAPO JUU NA UONGOZI WA SHULE***

…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………

JINA LA MZAZI……………………………………… SAHIHI……………………………